**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, (TaSUBa)

**KANUNI NA SHERIA NDOGONDOGO ZA MWANACHUO (Student By-Laws)**

**FEBRUARI, 2024**
**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, (TaSUBa)

**KANUNI NA SHERIA NDOGONDOGO ZA MWANACHUO (*Student By-Laws*), 2024**
*(Zimeundwa chini ya Aya ya 3, Aya ndogo ya 3.5 ya Sheria iliyoanzisha TaSUBa; TS. Na. 220/2007)*

Ninaidhinisha
**Mkuu wa Chuo**

***Sheria Ndogondogo za Mwanachuo ya maadili mema na ya kuzingatia mafunzo kwa ufanisi na taaluma bora.***

**UTANGULIZI**

KWA KUWA TaSUBa imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245 kupitia Tangazo la Serikali Na. 220/2007 kwa malengo ya kutunza, kuendeleza na kukuza Sanaa na Utamaduni wa Tanzania.

NA IJULIKANE Kuwa Taasisi ili kufikia malengo yake ina jukumu la kufanya utafiti, kutoa huduma ya ushauri na kufanya mafunzo kwa vitendo na nadharia katika maeneo ya Sanaa na Utamaduni,

NA IELEWEKE Kuwa Taasisi inaweza kutekeleza majukumu na kufikia malengo yake pale tu kuna mazingira salama na wezeshi yenye amani na utulivu ya kutolea mafunzo ili kuendeleza uhuru wa fikra na kujieleza kwa kuheshimu wengine,

NA KWA KUTAMBUA Mamlaka za Menejiment kupitia sheria iliyoanzisha Taasisi ya kutunga na kuweka Miongozo, Kanuni na Taratibu ya kuweza kusimamia Taasisi ili ifikie malengo yake katika hali ya amani,

KWA HIVYO BASI, Bodi inapitisha Kanuni na Sheria hizi Ndogondogo za Mwanachuo ili kuweka mazingira ya wazi na haki kwa wote ya kuwasimamia Wanachuo na Taasisi kuweza kutekeleza majukumu yake na kulinda heshima ya Taasisi.

**Unukuzi;**

Kanuni na Sheria hizi Ndogondogo zitanukuliwa kama Sheria Ndogondogo za Mwanachuo *(Student By-Laws)* wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo za mwaka 2024.

**Matumizi;**

Kanuni na Sheria hizi Ndogondogo za Mwanachuo zitatumika kwa Wanachuo wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo na zitaanza kutumika rasmi zitakapoidhinishwa na Menejimenti na kupitishwa na Bodi ya Ushauri na kutangazwa kupitia Tovuti ya Taasisi.

**Tafsiri;**

*"Chuo":* Inamaanisha Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, maana sawa na TaSUBa.

*"Eneo la Chuo":* Inamaanisha maeneo ya yote ya Chuo ambapo Chuo kinaendesh mafunzo ikiwa ni Pamoja na maeneo ya Makazi ya Wanachuo.

*"TaSUBa":* Ina maana sawa na ya Chuo.

*"Mwanachuo":* Inamaanisha yeyote aliyedahiliwa kuwa mwanafunzi halali katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ikimjumuisha pamoja na mwanachuo wa kozi fupi.

*"Kamati ya Nidhamu":* Inamaanisha Kamati ya Nidhamu iliyoundwa chini ya kifungu cha 44

*"Mkuu wa Chuo":* Inamaanisha Mkuu wa Chuo au Kaimu wake.

*"UwaTaSUBa":* Inamaanisha Serikali ya Umoja wa Wanachuo TaSUBa.

*"Mwadili":* Inamanisha Mkufunzi aliyeteuliwa na Menejimenti kuwasimamia na kuwalea Wanachuo.

*"Kampasi":* Inamanisha Tawi lolote la TaSUBa mahala popote.

*"Mabweni ya Chuo":* Inamaanisha Eneo lilotengwa na Chuo kama sehemu ya Makazi ya Wanachuo Maana sawa na Hostel.

*"TS":* Inamaanisha Tangazo la Serikali.

*"Baraza":* Inamaanisha Mkutano wa Wanachuo wote na uongozi wa Chuo.

*"Mamlaka ya Nidhamu":* Inamaanisha Naibu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala au Afisa yeyote aliyekasimiwa madaraka ambaye atafanya kazi kwa pamoja na Jopo la Ushauri kama ilivyoundwa chini ya kifungu cha 44.

*"Mamlaka ya Rufaa":* Inamaanisha Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanachuo iliyoundwa kupitia kifungu cha 61 cha Sheria hizi.

*"Ada ya Masomo":* Ni ada anayopaswa kulipa mwanachuo ili kupewa mafunzo na ni pamoja na mchango halali wa uwanachama wa *UwaTaSUBa.*

*"NACTVET":* Inamaanisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

*"Chumba":* Inamaanisha Chumba au sehemu aliyopangishiwa Mwanachuo katika Mabweni ya Chuo kwa ajili ya kuishi.

## SURA YA KWANZA

MASHARTI YA UDAHILI WA MWANACHUO

1. Kudahiliwa kwa mwanachuo yeyote kunategemea na mwombaji kukubaliana na masharti yafuatayo:

   (a) Kukubali, kuheshimu na kutii Sheria Ndogondogo hizi za Mwanachuo, Miongozo mingine pamoja sheria za Nchi.

   (b) Malipo ya ada za mafunzo ndani ya muda uliowekwa na uongozi.

   (c) Kuheshimu na kutii uongozi wa Chuo, wafanyakazi, Serikali ya Umoja wa Wanachuo pamoja na kila mwanachuo.

## SURA YA PILI

HAIBA.

2. Kila Mwanachuo atatakiwa kuvaa mavazi ya heshima muda wote akiwa ndani na nje ya chuo. Aidha Wanachuo wa kiume itakuwa marufuku kuvaa suruali kwa nusu makalio na wanawake kuvaa sketi fupi zilizo juu ya magoti, vitovu wazi na nguo zinazo acha kwapa wazi na sehemu kubwa ya vifua wazi na nguo za kubana na kuonesha sehemu na viungo vya ndani ya mwili.

3. Mwanachuo atatakiwa kuvaa *truck suit* au nguo ya heshima isiyobana na kuonesha sehemu na viungo vya ndani ya mwili na awe na kitambulisho muda wote awapo katika eneo la chuo na kwamba ataruhusiwa kuvaa vazi la somo awapo katika shughuli za somo husika.

4. Ni marufuku kwa mwanachuo kuvuta sigara, kunywa pombe au kilevi chochote madarasani au katika eneo lolote la kutolea mafunzo au popote na kupelekea kuathirika kwa majukumu ya Taasisi.

5. Ni marufuku kwa Mwanachuo kutumia au kuwa na bangi au aina yoyote ya madawa ya kulevya.

## SURA YA TATU

HESHIMA, UTII NA UADILIFU

6. Kila Mwanachuo atatakiwa kujiheshimu, kuwaheshimu wenzake, kuheshimu uongozi wa Chuo, Serikali ya Wanachuo, watumishi wote wa Taasisi na kila mtu.

7. Kila Mwanachuo atatakiwa kutunza muda na kuwahi na kuwepo mahali popote atakapohitajika hususani darasani na katika vikao mbalimbali hapa chuoni.

8. Ni marufuku kwa mwanachuo kujiingiza katika tabia za uzinzi na uasherati.

9. Ni marufuku kwa mwanachuo kufungulia sauti ya juu redio au Runinga au kifaa chochote kile cha kutoa sauti awapo bwenini au katika maeneo ya kujisomea.

10. Hairuhusiwi kwa Mwanachuo yeyote kukaa au kuwepo nje ya chuo zaidi ya saa 6.00 usiku kwa wanaoishi katika mabweni ya Chuo isipokuwa kwa kibali maalumu.

11. Ni marufuku kwa Mwanachuo kuiba au kutapeli au kutumia udanganyifu wa aina yeyote ile.

12. Hairuhusiwi kwa Mwanachuo kupigana hadharani au kwa kificho, kutoa lugha chafu, kutukana na kutishia usalama au amani ya mtu au kuonesha ishara yoyote ile inayochochea fujo.

13. Ni marufuku kwa mwanachuo wa jinsi tofauti kuingia katika bweni la jinsi nyingine baada ya saa 04:00 usiku

14. Ni marufuku kwa Mwanachuo kwenda nyumbani kwa mtumishi wa chuo pasipo idhini kutoka kwa mtumishi husika.

15. Kila mwanachuo anawajibu wa kulinda mali yake binasfi, ya chuo na ya umma.

16. Kila mwanachuo atatakiwa kuzima simu au kuweka kwenye mtetemo awapo darasani, Maktaba au kwenye kikao.

17. Kila panapokuwa na kikao kila Mwanachuo anatakiwa kusaini mahudhurio juu ya kuwepo kwake.

18. Kila mwanachuo atatakiwa kusaini fomu maalum wakati wa kumaliza masomo ya Muhula ili kuhakiki kama amerejesha mali yoyote ya chuo mahali husika.

19. Ni marufuku kwa mwanachuo yeyote kumbagua mwenzake kwa sababu zozote zile za kirangi, utaifa, jinsi, afya, ukabila au mahali anapotokea, mwelekeo wa kidini, ulemavu, umri, au hali ya maisha yake.

## SURA YA NNE

MAWASILIANO

20. Kila mwanachuo atatakiwa kufuata ngazi katika hatua zote za kutatua matatizo ambazo ni kuanzia Serikali ya Wanachuo mpaka ngazi ya Utawala wa Chuo kuanzia kwa Mwadili.

21. Ni marufuku kwa Mwanachuo kuandika maandishi au kubandika aina yoyote ya tangazo au maandishi katika kuta au majengo au katika mali yoyote ya Chuo.

22. Mawasiliano yote ya kutumia mbao za matangazo ni lazima yathibitishwe na Mwadili kabla ya kubandikwa na kwamba Waziri wa Habari ndiye atakayehusika na uandaaji wa matangazo kwa upande wa UwaTaSUBa na kuidhinishwa na Afisa Habari wa Chuo.

23. Mawasiliano yote kwa njia ya maandishi kutoka kwa Serikali ya UWATaSUBa yanatakiwa yapitie kwa Mwadili na Afisa Habari wa Taasisi.

24. Mwanachuo yeyote haruhusiwi kutumia nembo ya Chuo bila kibali maalumu.

## SURA YA TANO

USAFI, ULINZI NA AFYA

25. Ni marufuku kwa Mwanachuo kula chakula mabwenini/hostel.

26. Ni marufuku kupika chakula au kumiliki vyombo vya upishi mabwenini.

27. Kila Mwanachuo atatakiwa kufanya usafi katika chumba chake mara kwa mara pamoja na kufuata ratiba ya usafi iliyowekwa.

28. Kila mwanachuo mwenye gari au chombo chochote cha kusafiria na kuileta katika eneo la Chuo anawajibu wa kutoa taarifa kwa uongozi kwa njia ya maandishi na kuthibitisha umiliki wake na atawajibika na ulinzi wa mali yake.

29. Kila Mwanachuo anapaswa kuwa na bima ya afya.

30. Kila Mwanachuo anatakiwa kushiriki shughuli za michezo kila Ijumaa kuanzia saa 10:30 – 12:00 jioni na kwa siku ya Jumamosi itakuwa ni siku ya usafi kwa wanachuo wote kuanzia saa 12:00 – 04:00 asubuhi.

**SURA YA SITA**

MASHARTI MENGINE

31. Kila mwanachuo ana haki ya kuomba chumba katika mabweni ya Chuo na kukilipia kodi kwa kuzingatia kiasi na utaratibu uliowekwa na Taasisi pamoja na kusaini Mkataba wa Upangishi. Si lazima kwa kila mwombaji apate chumba kwa kuwa nafasi ni chache na kipaumbele watapewa waombaji wasiojiweza na wanachuo wa Mwaka wa kwanza. Chumba kitaombwa kwa kila mwaka wa masomo na kutolewa kwa Mkataba wa muhula mmoja wa masomo isipokuwa kwa sababu maalumu na kwa kibali cha uongozi wa Taasisi.

32. Kila mwanachuo atakayepewa chumba katika Mabweni/Hostel za Wanachuo anawajibu wa kusaini na kuheshimu Mkataba wa Upangishi na Chuo.

33. Kila mwanachuo aliyedahiliwa katika Taasisi ni mwanachama wa umoja wa wanachuo kwa kuzingatia Katiba ya umoja huo iliyothibitishwa na Utawala wa Chuo.

34. Wanachuo wote wa kozi fupi na ndefu watatakiwa kulipa ada ya uanachama wa UwaTaSUBa kabla ya kuanza masomo.

35. Kila mwanachuo anatakiwa kukubaliana na kutii taratibu na miongozo iliyopo na kadri itakavyotolewa na NACTVET.

36. Kila Mwanachuo anatakiwa kuzingatia na kufuata Taratibu na Kanuni zote za chumba cha mtihani.

37. Ni marufuku kufanya vitendo vya udanganyifu katika chumba cha mtihani. Mwanachuo atakaye bainika akifanya udanganifu katika chumba cha mtihani atawajibika kwa mujibu wa Taratibu za Mitihani zilizopo.

38. Kila Mwanachuo anao uhuru wa kuabudu dini yoyote kutegemeana na imani yake na kuheshimu imani ya mwingine.

39. Makosa ya kinidhamu na adhabu husika yameainishwa katika Jedwali la Kwanza la sheria hizi.

**SURA YA SABA**

SEHEMU YA KWANZA

MAKOSA YA NIDHAMU KWA UJUMLA

40. Kwa madhumuni ya Sheria Ndogondogo hizi za Mwanachuo na bila kuathiri kifungu kingine ndani ya sheria hizi na sheria za Nchi, yafuatayo ni makosa ya kinidhamu:-

(a) Kitendo ambacho kinaweza au kusababisha fujo au uharibifu wa mali ya Chuo au ya mtu binafsi nje au ndani ya Chuo.

(b) Kutumia nguvu, fujo, tishio au mgomo dhidi ya mtumishi yeyote wa chuo au mwanachuo.

(c) Kuharibu au kuteketeza kwa hila mbaya mali yoyote ya Chuo au ya mwanachuo.

(d) Kitendo ambacho kinaweza kukwamisha shughuli halali za kitaaluma au kiutawala au vyote kwa pamoja.

(e) Matumizi ya kiufundi au huduma yeyote ile bila kibali maalumu.

(f) Kumiliki visivyo halali ufunguo wa ofisi au mali yoyote ya Chuo.

(g) Kukataa au kushindwa kutii amri au agizo au maelekezo halali yaliyotolewa na kiongozi yeyote wa Chuo au kwa niaba yake.

(h) Kutoa taarifa ya uongo kwa kujua au ya kutoaminika na kuonekana kuwa za kweli.

(i) Kutumia lugha au maneno machafu au ya kutishia dhidi ya mtumishi wa Chuo, mwanachuo au mtu yeyote katika mazingira yoyote.

(j) Kughushi nyaraka yoyote kwa dhumuni la kusababishia hasara chuo, mwanachuo au mtu yeyote.

(k) Kualika au kuendekeza wanachuo ambao majina yao yapo katika ubao wa matangazo na wamezuiwa au kukatazwa kuonekana katika mazingira ya chuo.

(l) Kukaidi, kukataa au kushindwa kutii amri au maagizo halali yaliyotolewa na Kamati ya Nidhamu au Kikao chochote halali cha Chuo.

(m) Kitendo chochote chenye lengo la kukwamisha shauri au mwenendo wa shauri la kinidhamu inayoendelea mbele ya kamati ya nidhamu au Mamlaka ya Rufaa au mamlaka yoyote ya Chuo au kumkwamisha shahidi kutoa ushahidi wake mbele ya Mamlaka ya nidhamu.

(n) Kubadilika kuwa shahidi adui au kukataa kutoa ushahidi au kujibu swali au kielelezo au kitu chochote kinachohitajika kutolewa mbele ya kamati ya nidhamu.

(o) Kukaidi, kudharau au kushindwa kutii na kutekeleza amri, maamuzi au adhabu iliyotolewa na Mamalaka ya Nidhamu au mamalaka yoyote Chuoni.

(p) Kuitisha au kuhudhuria Mkutano au Baraza isiyohalali.

(q) Kumwalika mtu yeyote kutoka nje ya Chuo kama mgeni rasmi au mwenye kutoa burudani chuoni bila kibali maalum kutoka kwa uongozi wa Chuo.

(r) Kuandika au kutoa maneno kwa nia ya kumchafua mtumishi wa chuo, mwanachuo kundi la wanachuo au mtu yeyote.

(s) Kuunda au kuanzisha kundi la wanachuo lenye lengo la kuwagawanya au kuweza kuwagawanya umoja wa wanachuo na kupoteza au kutishia kupotea amani.

(t) Kumdhalilisha kijinsia mwanachuo au mtu wa jinsi yoyote: kwa madhumuni ya Kifungu hiki udhalilishaji wa kijinsia ni pamoja na:-

(i) Utani, maneno au kitendo cha kijinsia,

(ii) Kulazimisha vitendo vya ngono,

(iii) Kueneza uvumi au taarifa za uongo kuhusu maisha ya kingono kwa nia ya kumchafua mtumishi au mwanachuo yeyote,

(iv) Kugusana kusikotakiwa kijinsia, ambayo ni pamoja na; kushikana, kukonyezana na kubusiana, kugusa sehemu za siri au sehemu zenye msisimko wa kimapenzi bila ridhaa au kwa ridhaa kwa jinsi inayofanana.

(v) Kuonesha picha, video au vitendo vya kingono,

(vi) Kuonesha au kuacha wazi sehemu za siri au zenye hisia au mvuto wa kimapenzi,

(vii) Kutumia madaraka au mamlaka kwa uwazi au usiri na kurubuni kingono au kuadhabisha kwa kukataliwa kingono,

(viii) Kueneza kwa maandishi au kwa kauli mawasiliano ya kuudhi au yenye asili ya kingono,

(ix) Kujaribu kubaka au kubaka,

(x) Kufanya mapenzi kwa kundi,

(xi) Kujihusisha na shughuli au biashara yoyote ya kingono/usagaji/ushoga

(u) Kutokutunza vizuri, kuharibu au kutumia vibaya fedha za mfuko wa umoja UWATaSUBa kutegemea na Katiba ya umoja huo.

(v) Kukusanya au kuchangisha fedha kutoka kwa mwanachuo yeyote au kikundi cha wanachuo kwa nia ya kuwezesha uvunjifu wa sheria hizi.

(w) Kumiliki silaha ya aina yoyote visivyo hahali ndani ya Chuo; Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno silaha ni pamoja na silaha ya moto, kisu, fimbo, panga, shoka, kitu chochote chenye ncha.

(x) Kuingia kwenye chumba cha mwanachuo mwingine bila idhini ya wahusika.

(y) Kugoma, kushawishi au kutishia wanachuo kugoma kuingia madarasani au kufanya shughuli yoyote halali.

(z) Kupanga, kushawishi au kuhudhuria maandamano au makundi yasiyo halali.

(aa) Kuiba au kukutwa na mali ya wizi.

(bb) Kutumia pombe saa za mafunzo na kupelekea utoaji wa mafunzo kuathirika.

(cc) Kuendesha biashara ya aina yoyote katika eneo la Chuo isipokuwa kwa kibali maalum.

(dd) Kujihusisha au kushirikiana na mtu au kundi la watu wanaojihusisha na biashara ya madawa ya kulevya.

(ee) Kutenda kosa la jinai chini ya sheria za Nchi.

(ff) Kumiliki, kunywa, kujidunga, kuvuta au kujaribu kunywa, kujidunga, kuvuta au kumywesha, kumdunga, kumvutisha mtu yeyote sumu au aina yoyote ya madawa ya kulevya.

(gg) Kukaidi au kushindwa kulipa deni halali la chuo baada ya kuharibu mali yoyote ya Chuo.

(hh) Kupiga kelele, kusumbua au kumshawishi mwingine kupiga kelele au kusumbua katika eneo la Chuo.

(ii) Kuvunja mlango au dirisha au sehemu yoyote katika jengo au eneo ambapo hairuhusiwi mtu kupita au kuingia na kuiba au bila kuiba.

SEHEMU YA PILI

MAKOSA YA NIDHAMU YANAYOAMBATANA NA MATUMIZI YA MAKAZI

41. Makosa yafuatayo yanaambatana na matumizi ya makazi ya wanachuo;-

(i) Kupangisha chumba kwa mtu asiyehusika.

(ii) Kutumia chumba kwa madhumuni tofauti na yaliyokusudiwa.

(iii) Kuishi katika chumba kimoja na mwanachuo wa jinsi tofauti.

(iv) Kushiriki kitanda kimoja na mtu mwingine.

(v) Kuwaruhusu, kuwaalika au kuwaendekeza wageni kutoka nje kutembelea chumbani.

(vi) Kuvuta sigara na/au kunywa kilevi cha aina yoyote ndani ya chumba.

(vii) Kufanya matendo ya kingono/usagaji/ushoga ndani ya chumba.

(viii) Kupika chumbani.

(ix) Kumruhusu mwanachuo wa jinsi tofauti chumbani baada ya saa 4:00 usiku.

(x) Kuwepo nje ya chuo baada ya saa 6:00 usiku.

(xi) Kuharibu au kubadilisha samani zilizoko ndani ya Chumba.

(xii) Kupeleka chumbani Friji, drier, freezer, cooker au kifaa chocho cha kupikia, kuchemshia au kupoozea.

(xiii) Kuacha chumba bila kukabidhi na kurudisha ufunguo na/au godoro na mali zingine za chuo baada ya muhula wa masomo kuisha.

(xiv) Kumkatalia kiongozi yeyote wa Chuo au mwenye kibali kuingia na kukagua chumba au kufanya matengenezo.

(xv) Kukataa, kuzembea au kuacha kukabidhi chumba kwa Utawala wa Chuo baada ya muhula wa masomo kuisha.

(xvi) Kuacha chumba katika hali ya uchafu.

(xvii) Kupiga kelele au kuweka vyombo vinavyotoa sauti katika sauti ya juu.

(xviii) Kuacha taa za umeme zikiwaka muda wa mchana au muda ambao hakuna hitaji.

(xix) Kutokulipa kodi ya chumba ndani ya muda uliokubalika.

(xx) Kuishi ndani ya chumba bila kusaini Mkataba wa Upangshi na Chuo.

## SEHEMU YA TATU

### MAKOSA YA NIDHAMU YANAYOAMBATANA NA MATUMIZI YA CAFTERIA

42. Makosa yafuatayo yanaambatana na matumizi ya Mgahawa wa Chuo;-

(i) Kuvuta sigara katika eneo la Mgahawa na kuwathiri wateja wengine.

(ii) Kuingia jikoni bila ruhusa.

(iii) Kuondoka na kifaa chochote kutoka eneo la Mgahawa wa Chuo.

(iv) Kwenda katika eneo la Mgahawa wa Chuo kwa mavazi yanayoacha wazi sehemu za kwapa na kifua bila sababu za msingi.

## SEHEMU YA NNE

### MAKOSA YA NIDHAMU YANAYOAMBATANA NA MATUMIZI YA MAKTABA

43. Makosa yafuatayo yanaambatana na matumizi ya maktaba ya Chuo;-

(i) Kuondoka na kitabu, gazeti au kifaa chochote bila ruhusa maalum.

(ii) Kupiga kelele au kutumia simu kwa sauti ya juu au kusumbua ndani ya Maktaba.

(iii) Kutokurudisha au kuchelewa kurudisha ndani ya muda kitabu au kifaa chochote kilichoazimwa.

(iv) Kuharibu au kuchafua kitabu au kifaa chochote ndani au nje ya Maktaba.

(v) Kupoteza kitabu au kifaa chochote cha maktaba kilichoazimishwa.

**SURA YA NANE**

SEHEMU YA KWANZA

TARATIBU NA HATUA ZA AWALI ZA KINIDHAMU

44. (a) Kutakuwa na Mamlaka ya Nidhamu ya Wanachuo ambaye atakuwa Naibu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala au yeyote aliyekasimiwa madaraka hayo.

(b) Mamlaka ya Nidhamu ya Wanachuo itafanya kazi kwa pamoja na kwa kushauriwa na Jopo la Ushauri wa Nidhamu ya Wanachuo na itakaa kama Kamati ya Nidhamu ambayo wajumbe wake watateuliwa na Mkuu wa Chuo na kuidhinishwa na Manejementi kwa kuzingatia sifa zifuatazo:-

(i) Naibu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala (NMC/MFU)-ambaye atakuwa Mwenyekiti,
(ii) Mkuu wa Idara katika Ofisi ya Taaluma ambayo Mwanachuo mtuhumiwa anahusika-Mjumbe,
(iii) Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria-Katibu,
(iv) Mwadili:-Mlalamikaji,
(v) Afisa anayehusika na majukumu ya ulinzi katika Taasisi – mjumbe,
(vi) Wawakilishi wasiozidi wawili (02) kutoka Serikali ya Umoja wa Wanachuo - Wajumbe

(b) Maamuzi katika Kikao cha Nidhamu yatafikiwa kwa njia ya muafaka wa pamoja na endapo hakuna makubaliano ya pamoja, kura za siri zitapigwa na pale kura zitakapo lingana Mwenyekiti atakuwa na haki ya kura moja ya ziada.

(c) Akidi ya Kamati ya Nidhamu itakuwa si pungufu ya nusu ya wajumbe wote.

45. Mfanyakazi au mwanachuo au mtu yeyote anaweza kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Nidhamu ya Wanachuo pale ambapo kuna uvunjifu wa Sheria Ndogondogo hizi.

46. Mara baada ya kupokea taarifa ya uvunjifu wa sheria hizi, Mamlaka ya Nidhamu ndani ya siku mbili (2) za kazi atamwelekeza Mwadili kufanya uchunguzi wa awali ili kujiridhisha na tuhuma zilizowasilishwa kwake.

47. Endapo Mwadili katika uchunguzi wake atabaini kuwa hakuna uvunjifu wa sheria hizi au hakuna uthibitisho wa kutosha ataishauri ipasavyo Mamlaka ya Nidhamu pamoja na mtoa taarifa.

48. Endapo mtoa taarifa au mwathirika wa uvunjifu wa sheria hizi, hatakubaliana na ushauri wa Mwadili, atalipeleka lalamiko lake kwa maandishi moja kwa moja kwa Mamlaka ya

Nidhamu kupitia kwa Mwadili ambapo Mamlaka ya Nidhamu itajiridhisha kama kuna haja ya kuitisha kikao cha Kamati ya Nidhamu.

49. Endapo Mwadili katika uchunguzi wake atabaini kuwa kuna uvunjifu wa sheria hizi na kuna uthibitisho wa kutosha kuwa mtuhumiwa ndiye mhusika, atapeleka tuhuma kwa Mamlaka ya Nidhamu ili kuitisha kikao cha Kamati ya Nidhamu.

50. (i) Baada ya Mwenyekiti kupokea taarifa ya tuhuma, ndani ya siku mbili (2) za taarifa atamwandikia Taarifa ya Kikao na Hati ya Mashtaka mwanachuo mtuhumiwa.

(ii) Taarifa ya Kikao itaeleza siku, tarehe, muda na sehemu kikao kitafanyika na itatoa muda wa kujiandaa kwa mtuhumiwa usiopungua masaa 48 kabla ya Kikao cha Nidhamu.

(iii) Hati ya Mashitaka itaeleza jina la mwanchuo anayetuhumiwa, Namba za usajili, Kozi anayosoma, kifungu cha sheria hizi kilichovunjwa, siku, muda na mahali kosa lilipotendeka.

(iv) Endapo kosa la nidhamu lililotendeka pia ni uvunjifu wa sheria za Nchi na Mwanachuo husika amefikishwa mbele ya mahakama, basi taratibu za kinidhamu zitasimama na kusubiri maamuzi ya mahakama.

(v) Kama Mwanachuo mtuhumiwa wa kosa la nidhamu atafikishwa mahakamani na kuachiwa huru na mahakama kwa sababu za kiufundi kisheria, taratibu za kinidhamu zinaweza kuendelea dhidi ya Mwanachuo mtuhumiwa.

SEHEMU PILI

TARATIBU NA MWENENDO WA SHAURI LA KINIDHAMU

(51) Katika Kikao cha Kamati ya Nidhamu Mtuhumiwa atasomewa Hati ya Mashtaka na mtuhumiwa kutakiwa kujibu endapo anakiri au anakana tuhuma dhidi yake.

(52) Endapo mtuhumiwa hatahudhuria kikao cha Kamati ya Nidhamu kwa tarehe, siku na muda na mahali palipangwa na kuelekezwa katika barua ya wito;

(a) Kamati itajiridhisha endapo taarifa ya kikao hicho alipelekewa mtuhumiwa.

(b) Kama Kamati itabaini kuwa mtuhumiwa alipelekewa taarifa, itaendelea na shauri bila mtuhumiwa kuwepo na kulitolea maamuzi.

(c) Endapo Kamati itabaini kuwa taarifa hazikumfikia mtuhumiwa, itashauri kuwa taarifa kufikishwa kwa mtuhumiwa na kupanga tarehe nyingine ya kusikiliza shauri.

(53) Kama Mtuhumiwa baada ya kusomewa tuhuma dhidi yake;

(a) Atakiri kosa, Kamati itaendelea kutoa adhabu stahili kwa kuzingatia kifungu kilichovunjwa.

(b) Atakana kosa, Kamati itaamuru upande wa Mlalamikaji kutoa ushahidi.

(54) Baada ya upande wa Mlalamikaji kumaliza kutoa ushahidi, mtuhumiwa atapewa nafasi ya kuuliza maswali shahidi wa upande wa Mlalamikaji.

(55) Baada ya upande wa Mlalamikaji kumaliza kutoa ushahidi, Kamati itapima kwa kuzingatia ushahidi na vielelezo vilivyotolewa na kuamua kama Mtuhumiwa ana kesi ya kujibu. Endapo Kamati itaona Mtuhumiwa ana kesi ya kujibu itamtaka kutoa utetezi wake.

(56) Baada ya upande wa Mtuhumiwa kumaliza kutoa ushahidi, Mlalamikaji atapewa nafasi ya kuuliza maswali shahidi wa upande wa utetezi.

(57) Kamati itapokea ushahidi wa mdomo au wa vielelezo wakati wa kusikiliza tuhuma na pia inaweza kuhoji maswali mashahidi wa kila upande.

(58) Baada ya pande zote kutoa ushahidi, Kamati itatoa maamuzi yake ndani ya siku mbili (2) za kazi kwa kuzingatia ushahidi na vielelezo vilivyotolewa na kupokelewa na Kamati.

**SURA YA TISA**

SEHEMU YA KWANZA

ADHABU

(59) Mtuhumiwa akithibitika kutenda kosa la kinidhamu baada ya kusikilizwa na Mamlaka ya Nidhamu atapewa adhabu mojawapo au zaidi ya moja kwa pamoja kutegemea na uzito na marudio ya kosa kati ya: -

(a) Karipio kali,
(b) Onyo kwa Maandishi,
(c) Onyo la Mwisho,
(d) Kulipa fidia kwa Chuo au Mwathirika wa kitendo cha uvunjifu wa sheria hizi,
(e) Kurudisha mali yoyote iliyoibiwa.
(f) Kunyang'anywa na kuondolewa ndani ya chumba,
(g) Kunyang'anywa mali iliyopatikana kwa kuvunja sheria hizi.
(h) Kusimamishwa masomo kwa kipindi ambacho Mamlaka ya Nidhamu itaona inafaa lakini kisichozidi mwaka mmoja wa masomo.
(i) Kuzuiwa Cheti cha Taaluma au Hati ya Matokeo hadi adhamu itakapotekelezwa.
(j) Kufukuzwa Chuo.

(60) Endapo Mwanachuo atakutwa na kosa la kinidhamu ambayo adhabu yake ni kufukuzwa Chuo, Mwanachuo atakayefukuzwa Chuo hataruhusiwa kudahiliwa tena na Chuo mpaka baada ya miaka miwili kupita.

SEHEMU YA PILI

RUFAA

(61) Kutakuwa na Kamati ya Rufaa ya Nidhamu ya Wanachuo ambayo wajumbe wake watateuliwa na Mkuu wa Chuo na itakuwa na wajumbe wenye sifa zifuatazo:

(a) Mjumbe mmoja mwenye sifa ya Mkuu wa Idara kutoka Taasisi nyingine ya Mafunzo ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(b) Mjumbe mmoja kutoka Bodi ya Ushauri ya Taasisi.

(c) Mjumbe mmoja kutoka Ofisi ya Naibu Mkuu wa Chuo-Taaluma, Utafiti na Ushauri ambaye hajashiriki katika Kamati ya Nidhamu wakati kumsikiliza mtuhumiwa.

(d) Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria katika Taasisi ambaye atakuwa Katibu na hatakuwa na haki ya kupiga kura wakati wa maamuzi.

(e) Mjumbe mmoja kutoka Serikali ya UwaTaSUBa ambaye hajashiriki katika Kamati ya Nidhamu wakati kumsikiliza mtuhumiwa.

(f) Naibu Mkuu wa Chuo- Mipango, Fedha na Utawala ambaye atakuwa Mjibu Rufaa.

(62) Ambaye hataridhika na maamuzi ya Kamati ya Nidhamu ana haki ya kukata rufaa ndani ya siku kumi na nne (14) kwa Kamati ya Rufaa kwa njia ya maandishi akilieleza sababu za rufaa na atawasilisha Rufaa katika Ofisi ya Mkuu wa Chuo.

(63) Mkuu wa Chuo baada ya kupokea rufaa ndani ya siku saba (7) za kazi, ataitisha Kamati ya Rufaa na kumjulisha Mkata Rufaa siku, tarehe, saa na mahali Kamati ya Rufaa itakaa na kusikiliza Rufaa yake.

(64) Akidi ya Kamati ya Rufaa ya Wanachuo itakuwa si pungufu ya nusu ya wajumbe.

(65) Kamati ya Rufaa baada ya kupokea Rufaa inaweza kutia uzito na kukazia adhabu iliyotolewa na Kamati, kubadili na kutoa adhabu tofauti kati ya adhabu zilizotajwa kwenye kifungu cha 59 cha Sheri hizi au inaweza kuongeza, kupunguza au kuondoa adhabu.

(66) Si lazima kwa Kamati ya Rufaa kusikiliza tuhuma upya.

(67) Pale ambapo Mtuhumiwa atakata rufaa dhidi ya maamuzi ya Kamati ya Nidhamu, utekelezaji wa adhabu iliyotolewa na Kamati ya Nidhamu utaendelea mpaka majibu ya Rufaa yatakapotoka.

(68) Endapo Mwanachuo mtuhumiwa hataridhika na maamuzi ya Kamati ya Rufaa, atafuata taratibu kwa mujibu wa sheria za Nchi.

(69) Sheria hizi Ndogondogo na Mwanachuo zitafanyiwa mapitio muda wowote pale itakapoonekana inafaa kufanya hivyo kwa maslahi ya mafunzo bora na utawala bora.

Bagamoyo
Februari, 2024

Emmanuel M. Bwire
**Naibu Mkuu wa Chuo- Mipango, Fedha na Utawala**

## Jedwali la Kwanza

*(Chini ya Kifungu cha 39)*

## MAKOSA YA KINIDHAMU NA ADHABU

| | KOSA LA KINIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 1 | Kuwaalika au kuwaendekeza wageni kumtembelea mwanachuo chumbani. | Kupewa onyo kali au kunyang'anywa chumba au kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja. |
| 2 | Kumruhusu Mwanachuo wa jinsi tofauti kuwepo chumbani zaidi ya saa 4:00 usiku. | Kwa kosa la kwanza; Kupewa Karipio kali, kwa kosa la marudio; Kunyang'anywa chumba |
| 3 | Kuishi chumbani na mtu asiyehusika. | Kunyang'anywa chumba. |
| 4 | Kuharibu kwa makusudi au uzembe kifaa chochote cha Chuo ndani ya chumba. | Kunyang'anywa chumba au kulipa fidia ya uharibifu. |
| 5 | Kumwalika Mgeni kutoka nje ya chuo kama mgeni rasmi au mtoa burudani bila kibali maalum cha Chuo. | Kupewa onyo kali au kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja. |
| 6 | Kuacha taa ikiwaka muda wa mchana au pale ambapo hakuna hitaji ndani ya chumba. | Onyo la mdomo au kunyang'anywa chumba kwa marudio ya kosa zaidi ya mara mbili. |
| 7 | Kumiliki ufunguo wa wa chumba au kifaa chochote cha chuo bila kibali. | Onyo kali au kusimamishwa masomo kwa muda usiopungua mwaka mmoja. |
| 8 | Kukaidi au kuzembea kulipa deni la chuo kwa kupoteza au kuharibu mali ya chuo au deni lolote lililoripotiwa katika utawala wa Chuo. | Kumsimamisha mwanachuo mpaka atakapolipa deni husika. |
| 9 | Kuharibu mali ya chuo au ya mwanachuo mwingine kwa hila mbaya. | Kulipa fidia ya uharibifu na kupewa onyo kali na/au kumsimamishwa masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja. |
| 10 | Kutotunza vizuri au ubadhilifu wa pesa za mfuko wa wanachuo kutegemeana na Katiba husika. | Kulipa fidia, kupewa onyo kali na kusimamishwa masomo kwa kipindi cha mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| | | mmoja. |
| 11 | Kupokea au kukusanya kwa udanganyifu pesa kutoka kwa mwanachuo au mtumishi yeyote wa chuo. | Kulipa pesa zilizokusanywa na kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja. |
| 12 | Kufanya biashara ya aina yeyote katika eneo la chuo bila kibali. | Kupewa onyo kali na/au kusimamishwa masomo kwa kipindi cha mwaka mmoja. |
| 13 | Kitendo au maamuzi ambayo yatasababisha au kuweza kusababisha uhalifu au fujo dhidi ya mwanachuo au mtu mwingine yeyote katika eneo la chuo au mahala popote. | Kulipa fidia ya uharibifu na/au kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja. |
| 14 | Kutishia au kutumia fujo dhidi ya mwanachuo mwingine au mtumishi yeyote wa chuo. | Onyo kali na/au kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja. |
| 15 | Kufanya maandalizi au jaribio au kuitisha mkutano mkuu (Baraza) la wanachuo bila kibali. | Kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja au Kufukuzwa Chuo. |
| 16 | Kuandaa au kushiriki katika maandamano haramu. | Kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja au Kufukuzwa Chuo. |
| 17 | Kutoa taarifa za uongo kwa kujua kuwa ni taarifa za uongo. | Kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja |
| 18 | Kufanya vitendo ambavyo vinaweza kushawishi au kusababisha fujo baina ya wanacho dhidi ya mali yoyote au mtu yeyote mahala popote. | Kulipa fidia ya uharibifu, Kupewa onyo kali au kusimamishwa masomo kwa kipindi cha mwaka mmoja au kufukuzwa chuo. |
| 19 | Kukataa, kukaidi au kushindwa kutii amri au maelekezo halali ya Afisa wa Chuo au kwa niaba yake na kuathiri utendaji kazi wa Taasisi. | Kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja au Kufukuzwa Chuo.. |
| 20 | Kutumia maneno/kauli ya kumchafua mtu jina, au ya kuudhi au ya kutishia dhidi ya mwanachuo mwingine au mtu mwingine yeyote. | Kupewa onyo kali au Kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja au Kufukuzwa Chuo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21 | | Kutohudhuria au kukataa au kushindwa kuhudhuria kikao halali kilichoitishwa na uongozi wa chuo, Mamlaka ya nidhamu au uongozi wa Wanachuo pale ambapo kuna taarifa ya wazi katika ubao wa matangazo au kwa njia nyingine yoyote. | Kupewa onyo kali au Kusimamishwa chuo kwa kipindi cha mwaka mmoja au Kufukuzwa Chuo. |
| 22 | | Kukaidi au kukataa au kushindwa kutii na kutekeleza maamuzi au adhabu ya Mamlaka ya Nidhamu ya Chuo. | Kufukuzwa Chuo. |
| 23 | | Kujihusisha au kufanya au kuandaa shughuli zozote za kijamii katika eneo la chuo bila kibali. | Kupewa onyo la mdomo au kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja. |
| 24 | | Kuingia ndani ya chumba cha mwanachuo mwingine bila ruhusa ya mwenye chumba. | Kupewa onyo la mdomo au kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja. |
| 25 | | Kulewa na/au kufanya vitendo visivyo vya kimaadili kutokana na kilevi katika eneo la chuo au mahala popote pale na kuathiri majukumu ya Taasisi. | Kupewa onyo la mdomo au kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja. |
| 26 | | Kutumia nguvu, fujo au tishio au ukabaji dhidi ya mwanachuo mwingine au mtumishi au mtu yeyote ndani au nje ya eneo la chuo. | Kufukuzwa Chuo. |
| 27 | | Kitendo ambacho kinaweza kuzuia au kukwamisha au kutishia kutofanyika:-<br>(a) Vipindi madarasani au mazoezi ya vitendo,<br>(b) Kikao au shughuli halali ya chuo. | Kufukuzwa Chuo |
| 28 | | Kuunda au kuanzisha kikundi cha wanachuo ambacho inaweza kusababisha kupotea kwa amani chuoni au katika jamii. | Kufukuzwa Chuo. |
| 29 | | Udhalilishaji wa kijinsia wa aina yoyote. | Kupewa onyo la mdomo au kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja au Kufukuzwa Chuo. |
| 30 | | Kuitisha au kuhudhuria mkutano wa aina yoyote usio na kibali. | Kusimamishwa masomo mpaka muhula moja wa masomo. |
| 32 | | Kushitakiwa na Jamhuri kwa kosa lolote la | Kusimamishwa masomo mpaka kutolewa hukumu dhidi |

| | | |
|---|---|---|
| | kijinai, | yake, na kama atakutwa na hatia na kufungwa atafukuzwa Chuo. |
| 33 | Kutumia au kumiliki madawa ya kulevya. | Kufukuzwa Chuo. |
| 34 | Kulima au kustawisha au kutunza aina yoyote ya mimea yenye kulevya na iliyokatazwa na sheria za Nchi. | Kufukuzwa Chuo. |
| 35 | Kujihusisha au kushirikiana kwa hiari na mtu yeyote au kundi lolote ambalo linajihusisha na biashara ya madawa ya kulevya au aina yoyote ya vitendo vya kuvunja sheria za Nchi. | Kufukuzwa Chuo. |
| 36 | Kutumia au kumpatia mtu mwingine yeyote madawa ya kulevya kwa lengo au sababu yoyote ile. | Kufukuzwa Chuo. |
| 37 | Kumiliki silaha ya aina yoyote katika eneo la Chuo. | Kufukuzwa Chuo. |
| 38 | Kualika kwa hiari, au kuruhusu mwanachuo yeyote ambaye jina lake liko katika ubao wa matangazo na amekatazwa kuingia madarasani, au amesimamishwa masomo au kufukuzwa chuo. | Kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja au Kufukuzwa Chuo. |
| 39 | Kubaka | Kufukuzwa Chuo. |
| 40 | Kubaka kwa kundi. | KufukuzwaChuo |
| 41 | Kushawishi, kushiriki au kuandaa katika vitendo vya kuhatarisha amani kimakundi, kugoma kuingia madarasani, vikao, au shughuli yoyote halali ya Chuo. | Kufukuzwa Chuo. |
| 42 | Kuiba mali yoyote ndani au nje ya eneo la Chuo. | Kurudisha mali iliyoibwa au kufidia na kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja wa masomo au kufukuzwa Chuo. |
| 43 | Kughushi au kutumia nyaraka ya uongo kwa lengo la kulisababishia Chuo hasara au mtu yeyote. | Kusimamishwa masomo, Kufidia hasara na/ au kufukuzwa chuo. |
| 44 | Kujihusisha na biashara ya ngono katika eneo la chuo au nje ya eneo la chuo. | Kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja wa masomo. |

| | | |
|---|---|---|
| 45 | Kuvaa nguo isiyo ya kimaadili, malapa madarasani, maktaba bila kibali. | Onyo mara mbili na mara tatu kusimamishwa masomo mpaka muhula mmoja wa masomo. |
| 46 | Kufanya shughuli za kidini au kiimani katika namna au mazingira ya kukwamisha shughuli za chuo. | Onyo mara mbili na mara ya tatu kusimamishwa masomo kwa kipindi cha mwaka mmoja wa masomo. |
| 47 | Kufanya shughuli zenye itikadi za kisiasa katika eneo la chuo. | Kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja wa masomo au kufukuzwa chuo. |
| 48 | Kupangisha chumba katika mabweni ya Chuo kwa mtu mwingine yeyote. | Kunyang’anywa Chumba na kusimamishw kwa mwaka mmoja wa masomo. |
| 49 | Kutumia chumba katika mabweni kwa shughuli za kijamii bila kibali. | Kupewa onyo kali au kusimamishwa masomo kwa mwaka mmoja wa masomo. |
| 50 | Kuishi chumba kimoja na mwanachuo mwinigine wa jinsi tofauti. | Kunyang’anywa chumba na Kusimamishwa masomo kwa Muhula mmoja wa masomo. |
| 51 | Kumruhusu mtu wa jinsi yoyote kutoka nje ya chuo katika mabweni ya chuo zaidi ya saa 12:00 jioni. | Kupewa onyo au kunyang’anywa chumba. |
| 52 | Kunywa na kulewa, kuvuta sigara au kutumia kitu chochote ambacho kitapoteza amani kwa wengine katika eneo la chuo na kuathiri majukumu ya Chuo. | Kupewa onyo, au kunyang’anywa chumba au kusimamishwa masomo kwa kipindi kisicho pungua mwaka mmoja wa masomo. |
| 53 | Kupika chumbani au katika eneo la chuo. | Kupewa onyo au kunyang’anywa chumba. |
| 54 | Kuvamia au kuhamisha samani au mali yoyote ya Chuo bila kibali. | Kupewa onyo kali au kusimamishwa masomo mpaka mwaka mmoja wa masomo. |
| 55 | Kuleta ndani ya mabweni ya Chuo friji, drier, friza, au kifaa chochote cha kupikia. | Kunyang’anywa chumba na kulipa fidia ya matumizi ya umeme kadri itakavyokadiriwa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 56 | | Kumkatalia mfanyakazi yeyote wa chuo au mtu yeyote mwenye kibali kuingia chumbani na kufanya ukaguzi, au matengenezo au shughuli yoyote bila sababu za msingi. | Kunyang'anywa Chumba na kupewa onyo kali. |
| 57 | | Kuweka katika sauti ya juu Runinga, redio, Compyuta, au chombo au kifaa chochote kinacho toa sauti na kusababisha usumbufu kwa wakazi wengine. | Kupewa onyo kali au kunyang'anywa chumba. |
| 58 | | Kuondoka na kuacha chumba bila kukabidhi ufunguo na vifaa vingine kwenye uongozi wa Chuo. | Kulipia idadi za siku ambazo mwanachuo amebaki na ufunguo na kupewa onyo kali. |
| 59 | | Kuacha chumba katika hali ya uchafu wakati wa matumizi au kwenda likizo. | Kulipia gharama za usafi na kupewa onyo kali. |
| 60 | | Kuingia jikoni katika eneo la Cafteria na/au kuondoka na mali yoyote katika eneo la jiko. | Onyo kali na kurudisha mali na/au kusimamishwa masomo kwa kipindi cha mwaka mmoja wa masomo. |
| 61 | | Kuingia jikoni bila ruhusa. | Onyo la mdomo au la Maandishi. |
| 62 | | Kwenda Cafteria/Mgahawani na mavazi yasiyo ya kimaadili. | Onyo la mdomo kwa mara mbili, mara ya tatu kusimamishwa masomo kwa kipindi cha miezi mitatu. |
| 63 | | Kuondoka na kitabu, gazeti au kifaa chochote cha Taasisi bila kibali. | Kufukwa Chuo. |
| 64 | | Kupiga kelele au kutumia simu kwa sauti ya juu au kusumbua ndani ya Maktaba. | Onyo la mdomo au maandishi. |
| 65 | | Kuchelewa kurudisha ndani ya muda kitabu au kifaa chochote kilichoazimwa. | Onyo la mdomo mara mbili, mara ya tatu kunyimwa kuazimwa na kupewa onyo kwa maandishi. |
| 66 | | Kupoteza kitabu au kifaa chochote cha Maktaba kilichoazimishwa. | Onyo kwa maandishi na kulipia kitabu au kifaa na kutoazimishwa kitabu. |
| 67 | | Kurudia kosa zaidi ya mara moja | Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa ikiwemo kufukuzwa chuo. |